



Imani ni zaidi ya vitengo sabini au zaidi ya sitini, bora yake ni kauli ya Laa ilaaha illa Ilaah, na ya chini yake ni kuondoa udhia barabarani

Imepolelewa Kutoka kwa Abuu Huraira -Radhi za Allah ziwe juu yake- amesema:
amesema: Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-: "Imani ni zaidi ya vitengo sabini au
zaidi ya sitini, bora yake ni kauli ya Laa ilaaha illa Ilaah, na ya chini yake ni kuondoa
udhia barabarani, na haya ni sehemu katika imani".

[صحيح] [متفق عليه]

Anaeleza Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kuwa imani ina sehemu moja pamoja na mambo mengi, yanakusanya matendo itikadi na kauli. Nakuwa jambo la juu zaidi katika mambo ya imani ni kauli ya: Laa ilaaha illa Ilaah", kwa kujua maana yake, na kufanyia kazi matakwa yake, yakuwa Mwenyezi Mungu ndiye Mola Mlezi Mmoja wa pekee mwenye kustahaki kuabudiwa peke yake pasina mwingine zaidi yake. Nakuwa tendo dogo kabisa katika matendo ya imani ni kila chenye kuwaudhi watu katika njia zao. Kisha akaeleza - Rehema na amani ziwe juu yake- kuwa haya ni katika mambo ya imani, nayo ni tabia inayomsukuma mtu kufanya mazuri na kuacha mabaya.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/6468>

